**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA MKOA WA GEITA**

**MTIHANI WA MAANDALIZI KABLA YA MTIHANI WA UTIMILIFU**
**KIDATO CHA NNE**

# KISWAHILI

**MSIMBO: 021**
**MUDA : SAA 3** **MWAKA 2024**

## MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A,B na C zenye jumla ya maswali (11) kumi na moja.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B na maswali mawili (2) kutoka sehemu C. swali la 9 ni lazima.
3. Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
5. Andika namba yako ya mtihani katika ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

| KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU | | | |
|---|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **WEKA(V)** | **ALAMA** | **SAINI YA MTAHINI** |
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |
| 7 | | | |
| 8 | | | |
| 9 | | | |
| 10 | | | |
| 11 | | | |
| JUMLA | | | |
| SAINI YA MHAKIKI | | | |

## SEHEMU A (ALAMA 16)

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele [i]- [x] kisha andika herufi ya jibu hilo katika karatasi yako ya kujibia.

i. Hakuna sentensi bila kuwepo aina gani ya neno

A. Kielezi
B. Kitenzi
C. Kivumishi
D. Kiwakilishi
E. Nomino

ii. Ipi ni tofauti ya msingi kati ya Mashairi na Ngonjera?

A. Mpangilio wa Vina na Mizani
B. Idadi ya Vina na Mishororo
C. Majibizano baina ya watu wawili au zaidi
D. Mpangilio maalum wa Silabi na lugha ya Mkato
E. Mapigo ya kimuziki na ridhimu.

iii. "Ni budi nisome kwa bidii ili nifaulu mtihani wangu". Yapi ni masahihisho sahihi ya sentensi hii ?

A. Sio lazima kusoma kwa bidii ili nifaulu mtihani wangu.
B. Nina budi kusoma kwa bidii ili nifaulu mtihani wangu
C. Sitakiwi kusoma kwa bidii ili nifaulu mtihani wangu
D. Sina budi kusoma kwa bidii ili nifaulu mtihani wangu
E. Sio budi kusoma kwa bidii ili nifaulu mtihani wangu.

iv. Maneno yapi yameundwa kwa utohoaji

A. Duka na pima maji
B. Karoti na shamba
C. Namba na Kuku
D. Pikipiki na Papai
E. Chajio na chamcha.

v. Kwa kuzingatia kigezo cha kisintakisia unafikiri nomino jino inapaswa kuingia katika ngeli gani?

A. A-WA
B. KI-VI
C. LI-YA
D. U-YA
E. I-ZI

vi. Wewe u mdogo wangu, katika sentensi hii mofimu “u” hufanya kazi kama

A. Kiwakilishi
B. Kitenzi kishirikishi
C. Kiunganinishi
D. Kielezi
E. Kihusishi

vii. Maneno yapi kati ya yafuatayo yametokana na lugha ya kireno ?

A. Leso,meza,bendera
B. Doti,dobi,leso
C. Bakuli,pesa,bendera
D. Meza,leso,dobi
E. Beseni,meza,leso

viii. Kimapokeo,Nomino inayojitokeza upande wa kiarifu inaitwa

A. Kiima
B. Chagizo
C. Shamirisho
D. Kiarifu
E. Prediketa.

ix. Obogo alifurahi alipopata maswali yote ya Kiswahili.Neno lililopigiwa mstari ni…………

A. Nomino
B. Kielezi
C. Kitenzi
D. Kishazi tegemezi Kielezi
E. Kishazi tegemezi Kivumishi

x. Sentensi hii inatoka katika kundi la sentensi gani? Mwalimu ambaye ameondoka atarudi mwakani.

A. Sentensi ambatano
B. Sentensi sahilli
C. Sentensi tata
D. Sentensi changamani
E. Sentensi shurtia

2. Chagua kifungu cha maneno kutoka orodha "B" kinachotoa maelezo sahihi ya maneno katika orodha "A" Andika herufi ya jibu sahihi kando ya namba ya kipengele cha Swali katika karatasi ya kujibia .

| ORODHA „ A" | ORODHA „B" |
|---|---|
| i. Tangazo la taarifa<br>ii. Tangazo la uelekezaji<br>iii. Njia ya kutolea tangazo<br>iv. Muundo wa tangazo<br>v. Tangazo la tahadhari<br>vi. Matangazo rasmi | A. Huwa na kibali cha mamlaka husika<br>B. Usipite hapa<br>C. Malengo ya tangazo<br>D. Nafasi za kazi<br>E. Kuonesha walengwa<br>F. Tangazo<br>G. Huandikwa kwa herufi kubwa<br>H. Kichwa cha tangazo<br>I. Kufungua kata hapa<br>J. Bango |

**SEHEMU B (ALAMA 54)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii

3. (a) Lugha ya Kiswahili imetumia njia mbali mbali kuongeza msamiati wake, unadhani maneno yafuatayo yameongezwa katika lugha ya Kiswahili kwa njia ipi

i) Papai ii) Ombaomba iii) Tibu,buti iv) wachomoe

(b) Unda msamiati kwa kuambatanisha maneno yenye muundo ufuatao kwa kila neno

i)Nomino na nomino

ii) Kitenzi na nomino

iii)Nomino na Kivumishi

iv) Kitenzi na nomino

v) Nomino na kivumishi.

4. Ukiwa kama mwanafunzi uliyebobea katika uhakiki wa kazi za fasihi, onesha vipengele sita utavyozingatia katika kuhakiki muundo wa shairi.

5. (a) Kwa kutumia viambishi vya o-rejeshi ulizopewa hapo chini tunga sentensi moja kwa kila o-rejeshi. i) -cho- ii) -ye- iii) -lo- iv) -ko- v) -po-

   (b) Tofautisha uandishi wa Muhtasari wa kikao cha kwanza na muhtasari wa kikao cha pili kwa hoja mbili.

6. (a) Eleza maana ya usimulizi.
   (b) Fafanua kwa kina tofauti zilizopo baina ya usimulizi wa hadithi na usimulizi wa habari/matukio. Tumia hoja nne tu kuonesha tofauti hizo

7. Wewe ni askari wa jeshi la wananchi wa Tanzania ambaye umeteuliwa na askari wenzio kutamba majigambo katika sherehe ya kuadhimisha siku ya mashujaa.Tunga majigambo yenye beti nne utakayotamba siku hiyo ukionesha umuhimu na umahiri wako wewe askari.

8. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanafayofuata,

Hauchi, hauchi,unakucha. Sekunde zilipita na kuunda dakika.Nazo dakika zilipita zikawa saa. Saa zikaunganika na kufanya siku moja,mbili,siku ya tatu wanafunzi lufufu walijikuta wamo kwenye uwanja wa mashariki wa shule yao. Kila mmoja alikuwa kimya akisubiri kwa hamu muda wa kuchagua kiongozi ampendaye.Kiongozi wa uchaguzi alikuwa msaidizi wa mkuu wa shule akisaidiana na mwalimu wa nidhamu. Wagombea wawili wa nafasi ya kuwa kiranja mkuu waliitwa na kusimama mbele ya wanafunzi wote. Kila mmoja aliruhusiwa kutumia dakika tano tu kutoa maelezo mbele ya wapiga kura. Baada ya hapo kila mwanafunzi karatasi maalumu kwa ajili ya shughuli hiyo. Kwa kuzingatia kanuni za uchaguzi, kila mmoja alifanya alilotakiwa kufanya. Hatimaye mwalimu wa nidhamu kwa kutumia njia maalumu aliyoiandaa alikusanya karatasi zote za kura. Sijui ni nani atayepata wadhifa huo mzuri na wa kipekee kipindi hiki? Lilikuwa ni swali lililotawala wanafunzi wote muda wa kuchagua kiongozi wampendaye.

**Maswali**

i) Pendekeza kichwa kichwa cha habari uliyoisoma.
ii) Eleza maana ya ufahamu unaopatikana katika kifungu hiki cha habari.
iii) Kwa kuzingatia maarifa ya uliyopata katika mada za ufahamu kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne kifungu hiki cha habari ulichosoma kinapaswa kufupishwa kwa maneno mangapi ?
iv) Katika kifungu cha habari hii umetumia aina gani ya usomaji.
v) Fupisha habari uliyoisoma kwa sentensi tano tu.

**SEHEMU C (ALAMA 30)**

Jibu maswali mawili [02] tu kutoka katika sehemu hii.swali la 9 ni la lazima

**(ORODHA YA VITABU KWA SWALI LA 9-11)**

**USHAIRI.**

| | |
|---|---|
| Wasakatonge | - M.s Khatibu[ DUP] |
| Malenga wapya | - TAKILUKI [DUP] |
| Mashairi ya chekacheka | - T.A Mvungi [EP &D LTD] |
| **RIWAYA** | |
| Takadini | - Ben J Hanson[MBS] |
| Joka la mdimu | - E. Mbogo[HP] |
| Watoto wa mama N‟tilie | - A. J. Safari [hp] |
| **TAMTHILIYA** | |
| Orodha | - Steve Reynolds[MA] |
| Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe | - E. Semzaba [ESC] |
| Kilio Chetu | - Medical Aid foundation [THP]. |

9. Mwanamke katika tamthiliya mbili ulizosoma amekwezwa na kutwezwa. Thibitisha kauli hii ukionesha namna mwanamke alivyotwezwa. Toa hoja tatu kwa kila tamthiliya.

10. Waandishi wa Riwaya ya **WATOTO WA MAMAN'TILIE** na **JOKA LA MDIMU** wanaonesha sekta isiyo rasmi inakabiliwa na changamoto lukuki. Kwa kutumia hoja tatu kwa kila riwaya ulizosoma fafanua changamoto za sekta isiyo rasmi kwa mifano halisi.

11. Jamii za kiafrika zinakabiliwa na madhila kadha wa kadha, kama vile ukoloni mambo leo, ukeketaji mapenzi ya jinsia moja, matumizi mabaya ya pesa, Unyanyasaji wa kijinsia, Mapenzi ya uongo, michango holela katika dini/nyumba za ibada, mapenzi pesa/vitu na ufujaji wa mali za umma.Chagua madhila matatu kwa kila diwani kati ya yaliyotajwa hapo juu tu, kisha uthibitishe uwepo wa kila dhila kwa shairi moja moja.